# VITA 7 ZA KANISA LA MAHALA

# LAODEKIA

## VITA YA UVUGUVUGU

JAMES KALEKWA

# LAODEKIA:

## Vita ya Uvuguvugu

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo

MUKTADHA WA LAODEKIA ............................................. 5

KUHUSU UVUGUVUGU ..................................................... 9

Kwa nini Yesu anakemea uvuguvuguvu? .......................... 10

Uvuguvugu: *Mfano wa kumuua chura*.............................. 11

Uhalisia wa Waleodekia ................................................... 11

SABABU ZA UVUGUVUGU ............................................. 13

MADHARA YA UVUGUVUGU ........................................ 20

NAMNA YA KUSHINDA VITA YA UVUGUVUGU....... 24

Kuhusu Mwandishi: ............................................................ 26

Kuhusu New Vine Church: ................................................ 26

Mawasiliano na Mwandishi: ............................................... 27

## MUKTADHA WA LAODEKIA

Huu ni mji uliokuwa ni kitovu cha kibiashara ya Asia ya wakati huo. Palikuwa ni makutano ya watu kutoka maeneo mbalimbali ya ulimwengu. Kwa Tanzania, tungeweza kusema ni sawa na jiji la Dar es Salaam; ilikuwa ni kawaida kuona raia wa nchi za kigeni. Kwa sababu za kibiashara, Laodekia ilikuwa ni mji wenye huduma za kifedha kama vile benki, maduka ya kubadili fedha (bureau de change). Pia ulikuwa ni mji wenye huduma mbalimbali za chakula na malazi kwa ajili ya wageni wapitao kibiashara. Kwa sababu ya utajiri wa mtu mmoja mmoja na ule wa makusanyo ya kodi, mji wa Laodekia ulifahamika kama mji tajiri. Walikuwa ni matajiri kiasi kwamba mwaka 17 B.K kulipotokea na tetemeko kubwa sana lililouacha mji ukiwa umeharibika. Majengo yenye ufahari yalifutika na sifa yote ya mji kupotea. Mtawala wa dola ya Rumi alijitolea kuujenga upya mji

ule, lakini Walaodekia, kwa sababu ya ukwasi wao, walikataa kupokea msaada huo. Waliamua ya kwamba wataujenga mji wao wenyewe kwa fedha zao wenyewe.Na ndivyo ilivyokuwa. Ndani ya muda mfupi, Laodekia ilirudi kwenye utukufu wake wa awali.

Ni mji ambao ulikuwa na kituo cha utafiti wa afya kilichogundua dawa ya macho. Hii ni dawa iliyoihudumia dunia nzima kwa wakati huo. Ukitaka dawa ya macho, Laodekia ndiyo mahali pa kwenda.

Pia, mji huu ulifahamika kwa mavazi mazuri yatokanayo na manyoya ya kondoo wenye manyoya ya dhambara. Yalikuwa ndiyo mavazi daraja la kwanza ulimwenguni. Yalivaliwa na wafalme, wakwasi na watu wenye hadhi za kuheshimika. Ninadhani hata sasa twaweza kukubaliana, nchi ya Uturuki ni moja ya maeneo ambayo utapata mavazi yanayochukuliwa kwa hadhi ya umaalum ulimwenguni.

Uniruhusu nikuonyeshe kuhusu miundo mbinu ya mji wa Laodekia. Pamoja na utajiri wake wote lakini mji huu ulikuwa na changamoto kubwa sana ya maji. Hakukuwa na upatikanaji wa maji safi na salama kwa matumizi ya wanadamu;

hapakuwa na chanzo cha maji karibu yake. Hivyo viongozi wa mji walilazimika kuunda miundombinu ya kisasa ya kusafirisha maji kwa njia ya mabomba. Upande wa pili, jirani na mji huu kulikuwa na mji wa Kolosai – ule ambao waraka umeandikwa na mtume Paulo "Wakolosai" ambao ulikuwa na huduma nzuri ya maji yaliyotiririka kutoka kwenye barafu kali za milima iliyouzunguka mji. Kwa hiyo, wakolosai walifurahia huduma safi ya maji yasiyo na chumvi wala madini; safi kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote ile ya mwanadamu. Upande mwingine, Laodekia ilipakana na mji uitwao Hairepoli. Huu nao ulikuwa na chanzo kizuri cha maji ya chemchemi iliyokuwa ikichemka muda wote. Maji haya yalifaa kutumika kwa muda wote na wanadamu. (Wakolosai 4:13, 16)

Maji yaliyopatikana ndani ya mji wa Laodekia yalikuwa ni maji-chumvi; ilikuwa ni chumvi kali ambayo iliacha alama na mabaki ya madini chumvi kwenye vyombo vya kubebea au popote yalipotuama. Na zaidi ya yote, yalikuwa ni maji yasiyofaa kwa matumizi ya wanadamu. Mtu ambaye angeyajaribu kuyanywa, pindi anapoweka kwenye kinywa chake husikia kichefuchefu na humpelekea kutapika.

Kwa miundombinu ya kisasa (kwa wakati huo) utajiri wa Laodekia ulipelekea wavute maji kutoka kwenye vyanzo vyenye maji baridi. Ambayo yangewafaa kulingana na mazingira ya joto na hali yao ya hewa. Hata hivyo, yale maji baridi yaliyosafirishwa kwenye mabomba hayakufika yakiwa baridi… bali yakiwa kwenye hali ya uvuguvugu.

# KUHUSU UVUGUVUGU

*"Nayajua matendo yako, ya kuwa hu **baridi** wala hu **moto**; ingekuwa heri leo kama ungekuwa baridi au moto."* Ufunuo wa Yohana 3:15

Ukitazama utaona kuna lugha ya ulinganifu wa pande mbili kinzani – baridi na moto. Na kwa kuelewa zaidi utaona Bwana Yesu anaelekeza ya kwamba hupaswi kuwa vyote (baridi na moto), hupaswi kutokuwa vyote pia. Kwa makaripio hayo ya Yesu utafahamu ya kwamba, kimsingi unapaswa na unaweza kuwa kimojawapo – ama baridi au moto.

Sasa kwenye tafsiri halisi ya maneno hayo, kinachotumika siyo tu maneno baridi na moto bali inapaswa kusomeka kama baridi inayoganda au moto inayochemka. Kwa hiyo, hali inayozungumziwa hawa ni hali ya kuendelea kwenye upande huo. Siyo hali timilifu ambayo inaweza kurudi nyuma, bali hali timilifu inayoendelea upande huo. Kuna vitu vilivyoganda lakini vina uwezekano wa kurudi kwenye uvuguvugu; au vitu vilivyochemka ambavyo vinaweza kugeuzwa kuwa baridi. Hicho ndicho anachopingana nacho Yesu kwenye

kanisa hili na watu waliomo ndani yake. Kama mmeamua kuwa baridi basi muwe baridi inayoendelea kuwa baridi na isiyo na dalili ya kurudi nyuma; na kama mnakuwa moto basi muwe na moto unaoendelea kuchemka kwa uendelevu.

Kwa walaodekia onyo hili lilieleweka kwa urahisi zaidi… hali yao ya kiroho ilifanana nay ale maji yaliyosafirishwa! Kumbuka maji yalitoka kwenye chanzo cha baridi; na kwa ubaridi wake ndiyo yangefaa kutumiwa na watu kulingana na hali yao ya hewa… lakini yakawa kwenye uvuguvugu!

### Kwa nini Yesu anakemea uvuguvuguvu?

- Mifumo ya dunia hii haimwogopi mwamini mwenye hali ya uvuguvugu kwa sababu inafanana naye. – Hauwezi kukibadili kile unachofanana nacho na hauwezi kubadilishwa na kile unachofanana nacho.
- Adui atahakikisha ya kuwa mwamini anakuwa mtenda dhambi mstaarabu, yaani, anakuwa ni mwamini wa kwenda kanisani na kufuata taratibu zote za kanisa kama taasisi hakuna hakuna madhara yoyote.

## Uvuguvugu: *Mfano wa kumuua chura*

Wakati fulani nimewahi kumsikia mwalimu mmoja akifundisha namna ya kumuua chura bila chura kushtuka na kukimbia. Yule mwalimu alisema, ukimchukua chura na kumuweka kwenye maji ya moto ataruka mara moja. Anaweza kupata madhara kidogo lakini atakuwa sawa. Akasema, unaweza kuchukua maji yenye jotoridi linaloendana na chura husika; kisha maji hayo yakiwa ndani ya sufuria kubwa yawekwe kwenye jiko la mkaa na moto uwashwe. Chura atakuwa kwenye hali yake ya utulivu kwa sababu yumo kwenye mazingira aliyoyazoea. Hata hivyo, hatagundua ni lini hasa amekufa. Atakufa akiwa kwenye utulivu huo huo. Joto la maji litakapokuwa linabadilika, mwili wake utakuwa unabadilika kuendana nalo… mwishowe atakufa!

## Uhalisia wa Waleodekia

Watu wa kanisa hili waliuelewa sana ujumbe huu wa Bwana Yesu kwa sababu ya mazingira yao. Yesu alikuwa akiwaonya ya kwamba wamekubali kufanana na dunia; na huenda wamefika mahala pa kubadilishwa na dunia wakiwa wametulia na hawana la kufanya. Kama adui atayashambulia maisha ya mwamini

yeyote, hii ni njia mojawapo atakayoitumia kumshambulia.

# SABABU ZA UVUGUVUGU

Mambo yanayoleta hali ya uvuguvugu kwenye maisha ya mwamini na kanisa kwa ujumla na kama haya yanayoonekana kwenye kanis ala Laodekia.

1. Kufanya mali za dunia hii kuwa ndiyo lengo kuu na hitimisho *"Kwa kuwa wasema, **Mimi ni tajiri, nimejitajisirisha, wala sina haja ya kitu**; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi."* Ufunuo wa Yohana 3:17

Mpaka hapa ninaamini unakumbuka muktadha wa mji wa Laodekia. Mji wa kibiashara ambao unajitosheleza kimahitaji… kiasi cha kukataa msaada wa mtawala wa Rumi kuujenga mji ulipoanguka kutokana na tetemeko. Sasa, ndivyo lilivyokuwa kanisa la Laodekia na watu ndani yake. Walifika mahala pa kujitosheleza na kutokuwa na haja ya kitu… kiasi cha kutohitaji msaada wa Mungu kwenye maisha yao. Wanaomba nini kwa Mungu kama wana kila kitu? Wanamuhitaji Mungu kwa ajili gani iwapo wamejitosheleza na vyote?

Siyo tu kwamba mji na watu wa Laodekia ndiyo waliona mali za dunia hii kuwa ndiyo kila kitu kwao; bali hata kanisa lilifika kwenye kiwango hicho.

Kama kuna jambo huleta uvuguvugu kwenye maisha ya mwamini ni kufika mahala pa kugeuza kutafuta mali kama lengo kuu na hitimisho la maisha. Hii hupelekea kuona ya kwamba akipata kiwango cha mali alizokuwa nahitaji, basi ameyapata maisha… amepata vyote! Moyo wa mtu wa namna hii huhama kutoka kwa Mungu na kuzielekea mali za dunia hii.

Swali la kujiuliza na kujitathmini: ikiwa nitapata fedha, mali na milki zote…Je, bado nitaendelea kumuhitaji Mungu? Je, bado nitashikama na Mungu?

2. Kuweka tumaini kwenye uvumbuzi na/ au ugunduzi wa wanadamu *"Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajisirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini,* ***na kipofu****, na uchi. Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri,*

> *na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona."* Ufunuo wa Yohana 3:17-18

Yesu anaamua kuwadhihaki watu wa Laodekia kuwa wao ni vipofu! Lakini, si unakumbuka muktadha wao? Ulikuwa ni mji wenye kituo cha utafiti na tiba kilichogundua dawa bora ya macho kuwahi kutokea ulimwenguni.

Yesu anwaamsha kwa maneno makali kwa kuwaonyesha upofu wa matumaini yao. Kwa ugunduzi na utaalamu waliokuwa nao, walijiona kuwa hawatakaa waugue macho na/au wapofuke. Hiyo ni kuonyesha mahali tumaini lao lilipo!

Wakati ninakubaliana kabisa na uzuri na Baraka ya ugunduzi mbalimbali uliopo. Hata hivyo, tumaini libakie kuwa kwa Bwana Yesu pekee. Hata igundulie dawa yenye uhakikisho kiasi gani, lakini Bwana Yesu anabaki kuwa ndiye MPONYAJI!

Wakati mmoja tukiwa mahali fulani kwenye kambi ya kimisheni, mwanakambi mwenzetu (mchungaji) alipata jeraha mguuni. Akawa akiomba ya kwamba Mungu aingilie kati

kumponya. Kwenye kambi ile kulikuwa pia na watu kutoka Magharibi. Wao walibaki wakishangaa na kuhoji, *"Kwanini aendelee kuomba wakati sisi tuna dawa hapa?"*.

Ni rahisi sana kuangukia kwenye huo mtego na kuuhalalisha (justify). Kabla ya wao kuja na dawa, wanapaswa kujua huyu ndugu amekuwa na mtembeo wa namna hiyo na Mungu kuhusiana na afya ya mwili wake. Kati ya kutumia dawa na kuamini Mungu kukupa uponyaji… kutumia dawa ni rahisi sana! Sasa, sisemi ni dhambi kutumia dawa… nisemacho ni hiki, TUMAINI LIKO WAPI?

3. Dunia kujipenyeza kanisani – kuwa na dunia kanisani badala ya kuwa na kanisa duniani.

Kila tabia iliyokuwa inaweza kutumika kuuelezea mji wa Laodekia ndiyo ilikuwa inaweza kulifafanua kanisa la Laodekia. Kanisa na dunia walikuwa ni mapacha. Mojawapo ya jambo ambalo huupoza moto ndani ya kanisa ni pale ambapo kanisa litajaribu kuendana na dunia; na hasa lengo likiwa ni kutaka kukubaliwa na dunia. Kanisa limeitwa kuupindua ulimwengu siyo kuendana nao;

kanisa limeitwa kuukabili ulimwengu na siyo kukubaliwa nao. Kanisa ni nuru ya ulimwengu, limo duniani ili kumulika. Halipaswi kuuruhusu ulimwengu kulijaza kanisa. Ni kanisa duniani na si dunia kanisani!

4. Kuendelea na utaratibu na mifumo ya kidini hali Yesu akiwa nje ya kanisa na maisha ya mtu mmoja mmoja ndani ya kanisa *"Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja name."* Ufunuo wa Yohana 3:20

Kati ya jambo la mwisho kudhani kwenye kanisa ni kwamba Yesu yuko nje na waamini wamejifungia ndani. Jambo la ajabu sana kufikiria Yesu amesimama mlangoni anaomba kuingia kwenye kanisa lake! Mungu atuepushe mbali na jmabo hili.

Moja ya changamoto ya kanisa la Laodekia ni kugeuka kuwa kama chama cha ushirika. Walijisikia vizuri kubakia wenyewe tu. Hawakuhitaji mtu yeyote aongezeke kwenye "familia" yao. Huenda angewaharibia umoja au

ile hali ya kuzoeana baina yao. Lilikuwa ni kanisa lisilopokea wageni au watu wapya… maana yake walikuwa kinyume na agizo la Bwana Yesu. Hawakutaka watu waokoke na hawakutaka kuwafuasa waliookoka. Hakukuwa na nafasi hiyo! Kama kanisa halifanyi hao, linafanya nini sasa?

Si ajabu Yesu anabisha hodi mlangoni kwao ili ALE pamoja nao. Kwenye zama hizi za uandishi wa kitabu hiki kula ilikuwa ni zaidi ya kunawa mikono na kuanza kuchota chakula. Ilikuwa ni swala la ushirika zaidi. Ni mazungumzo na kufahamiana kwa kina. Kula kulichukua muda mrefu kwa sababu ya mkazo uliokuwa nyuma ya zoezi hili. Unakumbuka kanisa la kwanza kwenye kitabu cha Matendo ya Mitume ushirika wao ulidumishwa kwa "kumega mkate nyumba kwa nyumba" (2:46)… Yesu kama mwenyeji na mwenye (mmiliki wa) kanisa; na kama mgeni kwenye kanisa anaonyesha utaratibu wa kurudisha moto kanisani… ni kula pamoja! Ni kuwaendea walio nje, kuwaambia habari za Yesu, kuwafuasa na kuwa na ushirika nao. Lakini hiyo inaanza kwa kanisa kuwa na ushirika na Yesu.

Kwani wewe una ushirika na Yesu? Kwani wewe unatamani kuona wengine wakimgeukia Yesu, kufuaswa na kukua? Kama ni hapana… ni heri uwe moto leo!

# MADHARA YA UVUGUVUGU

Kwenye kila uvuguvugu tarajia kutakuwa na madhara. Na humo ndimo adui angetamani akufukishe na alifikishe kanisa. Kwa kilelezo cha kanisa la Laodekia, tujifunze.

1. Kutapikwa na Bwana Yesu – Mungu kutohusika na mambo yako, *"Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, **nitakutapika utoke katika kinywa changu."*** Ufunuo wa Yohana 3:16

Unayakumbuka maji yenye madini chumvi? Ambayo ukiyaweka mdomoni unajisikia kichefuchefu kiasi cha kutapika? Sasa, ndivyo ambavyo Mungu alikuwa analiona kanisa hili la Laodekia. Walikuwa wanatia kichefuchefu! Hitimisho la Bwana Yesu kuhusiana na watu vuguvugu ni kuwatapika watoke kinywani mwake.

2. Kuwa kinyume na mapenzi ya Bwana *"Mtu asiye pamoja name yu kinyume changu; na mtu asiyekusanya pamoja name hutapanya."* Mathayo 12:30

Kwenye kila juhudui waliyokuwa nayo Walaodekia. Yesu ameonekana wazi kabisa kuwa ndiye mpinzani wa kwanza na asiyekubaliana na kila wanalofanya. Siyo jambo moja – mambo yote yameonekana kutompendeza Bwana Yesu. Kama Yesu akiwa kinyume nami (detests) katika kila juhudi ninayoifanya, ni nani atakuwa upande wangu? Hata shetani hawezi kumsaidia mtu ambaye Mungu yuko kinyume naye. Sasa, hali ya uvuguvugu huvuta upinzani kutoka kwa Mungu mwenyewe. Atahakikisha amekupinga na amekukabili kwa maneno magumu na makali sana… *"kipofu, maskini, mnyonge, mwenye mashaka na uko uchi."*. Ninajua haya si maneno ungetamani kusikia kutoka kwenye kinywa cha Bwana wako.

Lakini hayo ndiyo huwatokea wale wanaoendelea kwenye maisha ya uvuguvugu.

3. Kukosa kuufurahia wingi wa msaada wa Bwana *"Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona."* Ufunuo wa Yohana 3:18

Bwana Yesu anaonyesha ya kwamba amejaa msaada tele kwenye kila eneo. Wakati walaodekia wanajidhania ni matajiri wasiohitahi kitu; wakati wanajidhania wao ni mji wa biashara uliojaa dhahabu; wakatiwanadhani mavazi ya kondoo yanawafanya wawe nadhifu na ugunduzi wa dawa ya macho utayahifadhi macho yao… Kumbe hawana kitu! Ni maskini, wako uchi, vipofu, ako uchi. Halafu kumbe Yesu amebeba jawabu la kila upungufu na uhitaji wao. Pamoja na utele na uwingi alioubeba Yesu kwa ajili yao, lakini wameshindwa kunufaika nao kwa sababu ya uvuguvugu wao… hawaoni mema pindi yanapoachiliwa.

4. Kutokuwa mtu wa matokeo (impact) *"Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajisirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi."* Ufunuo wa Yohana 3:17

Moja ya madhara yanayowapata watu vuguvugu kama lilivyokuwa kanisa la Laodekia ni kuwa na wasifu uliosheheni; kuwa na majina makubwa; kuonekana kuwa umejitosheleza… na kumbe yote hayo hayana maana yoyote kwako kwenye maisha ya sasa nay a umilele! Lakini vilevile

hayaongezi wala kupunguza chochote kwenye ufalme wa Mungu.

Ndio walikuwa na wingi na utele wa mali. Lakini zilifanya nini kuendeleza ufalme wa Mungu? Zilihusikaje kuwaleta wengi kwa Yesu? Ziliwasaidiaje kudumisha uhusiano wao wa karibu na Bwana Yesu?... Haikuwa na mguso wowote.

# NAMNA YA KUSHINDA VITA YA UVUGUVUGU

Ukiisoma barua hii iliyobeba ujumbe wa Bwana Yesu kulielekea kanisa la Laodekia. Utagundua ya kwamba haukuwa waraka wa laumu tu bali uliojaa masuluhisho kuhusiana na hali yao. Yesu anapenda sana kukusaidia kutoka kwenye hali ya uvuguvugu.

1. Mpatie Yesu Kristo nafasi stahiki kwenye moyo na maisha yako *""Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona."* Ufunuo wa Yohana 3:18

2. Kuishi maisha ya haki na usafi, *"Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri,* ***na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane****, na dawa ya macho*

*ya kujipaka macho yako, upate kuona."* Ufunuo wa Yohana 3:18

3. Kuweka vipaumbele na mkazo kwenye mambo ya rohoni na ya umilele *"Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona."* Ufunuo wa Yohana 3:18

4. Kuona kama Mungu anavyoona *"Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona."* Ufunuo wa Yohana 3:18

5. Kukubali na kupokea maonyo kwa unyenyekevu kama sehemu ya upendo wa Mungu kwako, *"Wote niwapendao mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidi, ukatubu."* Ufunuo wa Yohana 3:19

## Kuhusu Mwandishi:

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

## Kuhusu New Vine Church:

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

## Mawasiliano na Mwandishi:

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: James Kalekwa

Instagram: james_kalekwa

Youtube: James Kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-7764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

NEW VINE CHURCH *Dodoma*

# Abudu Nasi

**KILA JUMAPILI - saa 3.00 asbh -6.30 mch**

**KILA ALHAMISI - saa 11.00 jioni -12:15 jioni**



nvc_dodoma   +255 754 917 764

Mahali tulipo: **Swaswa - Njia Panda ya Waziri Mkuu**

*A Home of Impact*

## KUHUSU MWANDISHI



**James Kalekwa** ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake; ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; Baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa

james_kalekwa

@MchungajiJK

+255 754 917 764